

SIKAI

SIKAI

MUDDYB MWANAHARAKATI

Kimechapishwa na,
Fanani Mpole,
Dar es Salaam,
Tanzania.

Mobile: 0654-846-084

Mhariri: Mwl. Juma Nyange

: Mwl. Erick Gamba

Jalada: John Wisse

Msanifu kurasa: Muddyb Mwanaharakati

© Muddyb Mwanaharakati, 2020

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kinakili, kutafsiri, kupiga chapa au kukitoa kitabu hiki au sehemu yake kwa njia yoyote ile bila idhini ya Muddyb Mwanaharakati.

Chapa ya Kwanza 2020,

Mobile: 0713-538-427

ISBN: 978-9976-5467-2-9

FANANI MPOLE

DIBAJI

Nimesoma na kumaliza mkasa wa Sikai na Mwl Samweli.

Nimeona namna ambavyo baadhi ya walimu huchangia kufisha ndoto za mwanafunzi na kuwa kichocheo cha mtoto kuchukia shule.

Nimeona makundi rika [jinsi] yalivyo na nguvu ya ushawishi kama ilivotokea kwa Furaha alivyofanikisha kumwingiza Sikai kwenye uvuvi na utengenezaji wa mafyagio mpaka kupelekea kutaka kuiba baiskeli na [hatimaye] kukamatwa.

Lakini nimeona kwamba wapo baadhi ya askari wanaweza kushughulikia kesi kwa busara sana.

Nimependa katibu tawala alivojivika roho ya mzazi badala ya muhanga aliyetaka kuibiwa na kufanikisha Sikai kurudi shule.

Hanifa Kafashe
Morogoro,
Tanzania.
06/Oktoba/2020

SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Muumba wa ardhi na mbingu kwa kunipatia kipawa hiki. Pili kwa mama yangu mzazi kwa kunileta duniani. Mola akupe kauli thabiti huko uliko. Mwezi wa Julai, 2020, nilipata kuongea na John Wisse kuhusu kutunga kitabu cha watoto au vijana wadogo. Kauli yake ilikuwa “hatuwezi kufanya kazi ya kuandika mifupa iliyokomaa pekee bila kuwakumbuka mifupa miteke!”

Nilihamasika kwa kweli kwa kauli yake hiyo. Sikuona tena sababu ya kuishia njiani. Nikiwa katika hatua za awali kabisa, nikajikuta nikigawiana hadithi hii na baadhi ya marafiki zangu wa katika kundi sogozi la **READING MARATHON**. Rafiki huyo si mwingine bali Abby Shammy. Ulinitia moyo sana. Ulisema mengi kama mwalimu. Siwezi kusahau mchango wa Hanifa Kafashe. Ulinishauri, ulinipa njia na kukubali kuisoma katika muundo wake wa mwisho kabisa. Ahsante sana, Malkia wa Kiha.

Shukrani za pekee zimwendee mwalimu Juma Nyange kwa kuhariri kijitabu hiki. Hukunitupa! Ahsante sana. Shukrani ziwaendee Nawal Khalfan, Jamyl Kimoto na kaka Wisse kwa jalada zuri la kitabu hiki. Mchango wako kwangu utabaki moyoni mwangu milele.

Mohamed O. Lupinga (Muddyb)
Chanika, Dar es Salaam,
Tanzania.
12-Oktoba-2020

Katika mambo yanayomkera Sikai ni pamoja na kuamka asubuhi mapema kila siku za masomo ili aende shulenii. Siku ambazo haendi shule ni Jumamosi na Jumapili, hubaki nyumbani na kumsaidia mama yake kazi za nyumbani. Mama yake hukaanga mihogo kila siku kwa ajili ya kuuza ili apate pesa ya kupata mahitaji yake ya kila siku. Huamka mapema kuandaa vitu vyote vinavyotakiwa katika ukaangaji wa mihogo.

Mama Sikai, humwamsha mwanaye kila inapotimu saa kumi na mbili kasorobo asubuhi. Muda huo ndiyo hasa Sikai hujigezageuza kitandani kwa utamu wa usingizi na kiubaridi cha asubuhi.

“We Sikai, kushakucha amka tena mwanangu wende shule!” mama Sikai husema akimuamsha mtoto wake.

Sikai anasoma darasa la tatu. Ana umri wa miaka tisa. Awali alipenda sana kusoma. Moyoni alitamani aje kuwa daktari au rubani wa ndege. Kila siku alimwambia mama yake kuwa akiwa mkubwa anatamani kuwa rubani au daktari. Aliamini udaktari atawenza kuwasaidia wengi wenye shida mbalimbali za kiafya. Tangu asikie habari kuwa baba yake alikufa kwa ugonjwa wa kifua kikuu, hakupenda tena kuona mtu mwengine akifa kwa sababu ileile iliyochukua uhai wa baba yake.

Kwa upande wa urubani, alipenda sana kusafiri na ndege. Aliamini iwapo atakuwa rubani, basi ndoto yake ya kusafiri miji mbalimbali duniani itatimia.

Mama Sikai ambaye wengi walizoea kumwita Mama Mihogo hakuacha kumhimiza mwanaye kuhusu elimu. Mara nyingi alizoea kumwambia, "Kama kweli mwanangu una ndoto za kuwa rubani au daktari, basi ongeza juhudii katika masomo. Hakuna gumu ukiwa na elimu.

"Nitasoma, mama. Wala usihofu!"

"Basi vizuri, mwanangu!"

"Nitaushangaza ulimwengu, mama!"

"Kwa yakini, mwanangu!"

"We' niombee tu nisome kwa bidii!"

"Kila lenye heri likutangulie, mwanangu!"

"Ahsante, mama!"

Alitoka kitandani kwa kujinyonga mno. Hakuwa na chaguo badala isipokuwa kufuata maagizo ya mama yake. Akaenda **maliwtoni** huku akiweka mswaki wake mdomoni. Choo chao cha makuti, shimo la pipa, mlango wa kigunia. Wameegemeza mawe chini ili kuzuia upopo usifunue kigunia wakati mtu akiwa anajisadia.

Baada ya muda mfupi, alimaliza.

Akatoka akiimba wimbo aujuao yeye mwenyewe. Akarudi ndani, ambapo chumba chao ni kimoja tu. Wanalala pamoja na mama yake. Kuna kila kitu ndani. Madumu ya maji, jiko, ndoo za maji ya kunywa na makorokoro mengine mengi tu. Akatazama juu ya kamba, alining'iniza shati lake tangu jana yake usiku.

"Sikutaka tabu ya kulitafuta shati lilipo," Sikai alisema akilitungua shati juu ya kamba. Chini mchanga mtupu, nyumba yao haikuwekewa saruji kwenye sakafu. Si kwa kupenda, bali hali **duni** ya kimaisha imewafanya wafikie huko. Katika kazi ya mihogo, hakuweza kupata pesa nyingi za kukimu kula na kuendeleza shughuli za ujenzi.

Hata kibanda wanachoishi ilikuwa juhudzi za marehemu baba yake aliyejekuwa akifanya kazi ya ukuli bandarini, akafanya *ujanjaunja* wake wakapata kibanda cha udongo na paa la **tembe**. Maisha yakaendelea. Laitani baba yake Sikai asingelikuwa mtu wa kupenda pombe, pengine wangeishi katika nyumba iliyoezekwa bati na si tembe tena. **Kimfaacho mtu chake**, bado walijiona fahari kuwa na nyumba ya udongo na paa la makuti. Kwa sababu kero za kodi ziliwaepuka.

Sikai alitoka akaenda kando mwa chumba chao, kulikuwa na boksi analowekea nguo zake. Juu aliweka mfuko wake wa nailoni wenyewe madaftari ndani yake. **Akaunyakua** na kutoka mbio humo ndani. Manusura amvae mama yake aliyejekuwa nje akikaanga mihogo. Hakutazama nyuma tena, alijua kusimama kwake kungesababisha apigwe vibao.

Akiwa njiani, hali ya hewa ikabadilika.

Anga lilisusa kutoa mwanga unaostahili. Kukatokea dalili kamili za mvua. Sikai aliongeza mwendo. Kutoka nyumbani kwao hadi shulenii, ni mwendo wa kilomita mbili na nusu. Alipiga kasi zaidi kuepuka kulowa. Juhudi hazikuzaa matunda. Mvua ilianza kupiga kwa kasi sana. Sikai akatimua mbio kuelekea katika moja ya mikorosho mikubwa *iliyozongwazongwa* na kambakamba nyingi za mmea wa mlangamia. Humo alijificha na mvua haikumpata.

Akiwa chini ya mkorosho, akakuta wanafunzi wenzake watatu wakisubiri mvua ipite.

“Ah, Sikai! Sikai! Wahi upesi. Utaloa!” kijana aliyejekuwa amejificha chini ya mti asiloe na mvua alimwita kwa sauti Sikai.

“Aaah, Furaha! Umesimama muda mrefu hapa?”
Sikai alimwuliza mwanafunzi mwenzake.

“Hilo si swali, Sikai – ni jibu kabisa.”

“Pole sana, Furaha.”

“Pole wewe uliyechapwa na mvua.”

“Muda ushatutupa mkono. Mwalimu Samweli ni mkali sana. Huenda akatupiga kwa kuchelewa kwetu.”

“Sikai, hatuwezi kwenda na mvua. Sio salama. Isitoshe, madaftari yako yatalowa hayo.”

“Furaha, ni bora nilowe kuliko kuzipata fimbo za mwalimu Samweli. Hajui kupiga polepole yule. Kwa herini.” Sikai alitoka mbio na mvua yake. Hakujali kulowa kwa madaftari wala nguo zake alizovaa. Mvua haikumwonea huruma. Ilimchapa kwa kadiri itakavyo. Alifika lango kuu la shule huku moyo ukimwenda mbio. Akakimbilia upesi, **akajitoma** ndani.

Alivyofika nje ya darasa lake, akajikung’uta maji sana. Akavua shati lake, akalikamua maji yote kisha akalivaa tena. Akatazama mfuko wake wenye madaftari, angalau yalikuwa salama. Yalilowa kiasi tu kutokana na mfuko wake kuwa nailoni. Akajikung’uta kwa mara ya mwisho kisha akaingia darasani.

Alimkuta mwalimu Samweli akifundisha.

Akapita mbio kwenda kujificha katika madawati ya nyuma.

“Sikai, toka huko nyuma na uje hapa mbele!” mwalimu Samweli alisema akiwa anaandika ubaoni. Mwalimu Samweli ni mwalimu wa somo la hesabu. Somo analolipenda Sikai, lakini ajabu mwalimu wake hana mapenzi na Sikai. Humwona mchafu, hana unadhifu, kila wakati hunuka moshi. Pengine uduni wa maisha yake kwao kulalia kibatari, jiko la kuni hata utunzaji wa nguo zake

nyumbani kwao huwa ni mtihani. Utatunzaje wakati chumba chenyewe hicho-hicho ndiyo jiko.

“Inuka sijakwambia ukae.” mwalimu Samweli aliwaka.

Sikai akabaki wima kama alivyoagizwa. Mwalimu aliendelea kuandika hadi alipomaliza. Akamgeukia Sikai aliyesimama mithili ya mlingoti. Mwalimu Samweli akasogea hadi katika dawati lake la mbele akajiketisha juu yake huku mikono kaikunja akasema.

“Kwa nini umechelewa?”

“Kwa sababu ya mvua, mwalimu!”

“Mvua imeanza sasa hivi.”

“Imenikutia njiani, mwalimu.”

“Uliamka saa ngapi?”

“Mapema sana.”

“Si kweli. Usingechelewa.”

“Ni kweli, mwalimu.”

“Wacha maneno yako. Nyoosha mkono nikupige bakora zako kadhaa kisha ukaketi.”

“Nipige matakoni mwalimu. Mkononi hapana.”

“Usinipangie. Hebu nyooosha mkono.”

Sikai akajitahidi kunyoosha mkono lakini alichukua tahadhari kubwa. Hiyo tahadhari ndiyo iliyomponza hata akapigwa za mkono na nyingine za begani. Hakutoa sauti, kwa sababu kutoa sauti ni kuchochaea kipigo zaidi.

“Haya nenda kakae na uanze kuandika. Siku nyingine ukichelewa ni bakora tu – sitaki visingizio hapa.” mwalimu Samweli alisema akifoka. Huku akichua bega na mkono wake, Sikai aliondoka na kuketi dawati la nyuma kabisa. Mwalimu Samweli hakujali tena habari zake.

Alikaa darasani akafanya masomo yote aliyopaswa kufanya kwa siku hiyo. Wale akina Furaha na mwenzake hakuwaona. Akili ikamjia wasiwasi. Alipata kusikia habari za mvua na kukaa chini ya miti na hatari ya radi. Si kawaida yao kukosa kuwaona. Ijapokuwa mara chache huwa hawaonani. Akapata wazo la kuwatafuta. Akazurura viwanja vyote vya shule na asiwapate. Hatimaye akaazimia kurudi nyumbani bila kujua habari zao.

Akiwa njiani, katikati kutoka shule na kurudi nyumbani kwao, aliwaona akina Furaha wakiwa katika bwawa kubwa wakishika ndoo za plastiki walizotoboa kwa juu wakivua samaki aina ya kambale. Ni bwawa maarufu kijijini kwao. Lakini Sikai si mwepesi sana kushirikiana nao. Mama yake humtaka arudi mapema nyumbani ili kumsaidia kazi zake. Akili yake ikamtuma aende, lakini kuna sauti nyingine ilimkataza. Ilimuasa arudi nyumbani. Shauri la utoto likachukua mkondo mkuu. Sikai akasogea bwawani.

“Nyie akina Furaha! Furahaaa!” Sikai aliita huku akikimbia.

“Eeeh, Sikai. Njoo tuvve pelege na kambale. Vua nguo hizo uje.” Furaha alisema kwa furaha. Akamtia tamaa kijana mwenzake. Sikai bado aliendelea kusimama nje akifikiria.

“Mwenzako mwalimu Samwelii kanichapa kwa kuchelewa.” Sikai alisema.

“Huo ni ujinga wako.” Furaha alijibu.

“Ujinga wangu tena?”

“Ndiyo!”

“Kwa nini?”

“Leo ilikuwa siku nzuri ya kutega shule. Kwa kisingizio cha mvua. Yule mwalimu simpendi sana. Hupenda sana kutupiga. Sijui hana watoto kwake?”

“Usiseme hivyo, Furaha. Anajaribu kutufundisha adabu tu. Mi’ nafikiri hana nia mbaya.”

“Nani kakwambia?”

“Ni mawazo tu. Simfikirii vibaya.”

Furaha akaacha kuhamisha ndoo yake kila sehemu kwa minajili ya kupata samaki. Akafikiria jambo akiwa majini, akaona si kweli. Akatoka kabisa nje hadi alipo Sikai.

“Unajua wewe ni mjinga sana.” Furaha alisema huku akimtazama Sikai.

“Kwa nini, Furaha?”

“Kwanza mwalimu hakupendi. Kila siku anakupiga wewe tu. Na bado unakuwa upande wake. Vipi unaogopa atakupiga zaidi?”

“Hapana, Furaha. Mi’ nimechukulia kama sehemu ya adhabu tu kutoka kwa mwalimu na si kama naonewa.”

“Kwa hiyo hujui kutofautisha uonevu na adhabu si ndiyo?”

“Nisingependa kujibu swal lako, Furaha.”

“Basi kwa heri. Niwache nivue samaki. Nikauze nipate pesa ya kutumia shule kesho. Nikitoka hapa utanikuta mikoroshoni nikitungua mabibo. Ukimalizana na mama yako uje mikoroshoni tukufundishe ujanja. Umezubaa sana wewe!” Furaha alisema huku akirejea majini tena.

“Sawa. Nitajitahidi nije. Haya, kwaheri.” Sikai aliaga.

Alifika nyumbani alikuta mama yake keshamaliza kuuza mihogo na kazi nyingi zilikuwa zinaelekeea ukingoni.

“Oh jamani, mwanangu huyo. Karibu baba, karibu!” mama Sikai alimplaki mwanawe kwa furaha. Akamkumbatia. Akachutama kidogo na kumshika usoni huku akimfutafuta usoni.

“Habari za shule mwanangu?”

“Nzuri, mama.”

“Umekula nini leo?”

“Sijala chochote kile mpaka sasa.”

“Oh, nimekumbuka. Sijakupa pesa asubuhi.”

“Ndiyo, mama.”

“Hukuniambia mwanangu!”

“Nafikiri kwa sababu ya mvua. Nikaogopa kuchelewa – nisipigwe na mwalimu Samweli.”

“Oooh, jamani, mwanangu. Naamini hujapigwa huko shule eeh?” Sikai akanyamaza kimya kidogo. Akakumbuka fimbo za mwalimu Samweli, anajua akimwambia mama yake, huenda akaenda kuanzisha maongezi ambayo baadaye yatamwongezea zaidi bakora. Akaepusha shari.

“Hapana, mama. Sijapigwa kabisa!”

“Vizuri basi. Nenda kabadili nguo na uje uchukue vitumbua vyako nimekuwekea, mwanangu.”

“Sawa, mama!”

Sikai akatoka mbio hadi chumbani kwao. Akavua nguo upesi na kuzianika nje ili ziendelee kukauka. Hata juu halikuwa kali sana lakini si sawa na kuziacha ndani zikanuka **uvundo**. Akafakamia vitumbua kama hana akili nzuri. Akisukumia na chai huku akimtazama mama yake. Mama alimhadithia mwanaye hadithi mbalimbali za kitoto, akajikuta akisahau shida na madhila yote aliyopitia mchana wake. Wakacheka, wakafurahi na kujiona watu kati ya walichonacho. Kadiri siku zilivyokatika, ndivyo moyo wa kusoma kwa Sikai ulizidi kupungua. Kwani mateso yasiyo na sababu kutoka kwa mwalimu Samweli yalizidi maradufu. Walimu wenzake walifurahia adhabu alizokuwa akiwapa wanafunzi. Kuna siku aliwahi kufika shule

mapema kupita kiasi kilichomkuta Mungu pekee ndiye anajua.

“Sikai! We’ Sikai!” mwalimu Samweli aliita kwa hasira. Sikai akageuka kutazama sauti inatokea wapi. Akamwona mwalimu Samweli ndiye aliyekuwa akimwita. Akamsogelea. Alikuwa amejibanza katika kikuta cha darasa la tano A, ambapo mtu akipita katikati ya uwanja wa shule si rahisi kumuona. Basi tu almradi kumtia kovu la nafsi.

“Mbona huji kusalimia walimu wako?” mwalimu Samweli alifoka mithili ya mbogo.

“Sijakuona, mwalimu.”

“Hujaniona?”

“Ndiyo, mwalimu!”

“We’ mtoto una dharau sana. Sasa leo nitaikomesha hiyo dharau.” mwalimu Samweli akamvuta kwa nguvu. Mkononi alishika ufagio wa chelewa na kidumu cha maji, kwa kasi aliyomvuta, vikamponyoka. Akashindwa hata kusema kitu – kwani mwalimu Samweli alimshikilia *nganganga*.

“Leo utamwagia maji bustani yote peke yako. Ukimaliza ndiyo utaingia darasani.” mwalimu Samweli aliwaka. Kisha akamsukuma. Sikai chini akaenda.

“Ndiyo – nimekuelewa mwalimu.” Sikai aliitikia kwa unyonge. Hakuwapo wa kumsaidia. Majira aliyointia yalikuwa mapema sana. Aliingia saa kumi na moja na dakika arobaini na tano. Kiza bado kiliendelea kushika hatamu. Wakati huu Sikai alikuwa darasa la tano. Kipindi chote tangu akiwa darasa la tatu amekuwa mtu wa kupata shida kutoka kwa mwalimu Samweli.

Watoto wenzake wengi wanafahamu namna anavyopata mateso kutoka kwa mwalimu huyo.

